

**SHULE YA SEKONDARI THEMI HILL**

**MASWALI MIA MOJA (100)**

**KISWAHILI KIDATO CHA 1**

**APRIL 2020**

1. Eleza maana ya lugha
2. Vitamkwa ch, k, a,l,u, nao vinaweza Kaunda maneno kama (toa mfano ya maneno matatu.
3. Alfabeti za kiswahili hugawanyika katika sehemu kuu mbili zitaje
4. Eleza maana ya konsonanti
5. Taja dhima nne za lugha katika mawasiliano
6. Nini maana ya lugha fasaha
7. Taja misingi mitatu ya lugha fasaha
8. Nini maana ya Irabu
9. Neno matamshi linatokana na neno gani? Litaje
10. Eleza athari mbili za kutotumia lugha kwa ufasaha
11. Sauti za lugha hugawanyika katika sehemu kuu mbili zitaje
12. Taja ala mbili muhimu zinazohusika katika utamkaji wa maneno
13. Kiswahili sanifu kina konsonanti ngapi ?
14. Nini maana ya lafudhi
15. Toa mifano miwili ya lafushi za lugha ya kiswahili
16. Eleza tofauti iliyopo kati ya konsonanti na Irabu
17. Nini maana ya sarufi
18. Taja aina saba za maneno
19. Nini maana ya kivumishi
20. Taja aina kuu nne za Nomino
21. Eleza maana ya nomino dhahania
22. Nini maana ya vivumishi vya jina kwa jina
23. Toa mifan mitatu ya vivumishi vya jina kwa jina. (kwa kutunga sentensi)
24. Tunga senstensi mbili kwa kutumia vivumishi vya sifa
25. Nini maana ya viwakilishi
26. Taja aina nane (8) za vivumishi.
27. Viwakilishi hugawanyika katika aina kuu tisa zitaje.
28. Eleza maana ya vitenzi
29. Taja aina kuu tatu za vitenzi
30. Tunga sentensi tatu kwa kutumia vitenzi vishirikishi
31. Nini maana ya vielezi ?
32. Taja ina kuu tano za vielezi
33. Tunga sentensi kwa kutumia vitenzi visaidizi (sentensi 3)
34. Kwa kutumia vielezi vya mahali tunga sentensi tatu
35. Ainisha aina za maneno katika sentensi zifuatazo  
(a) Baba analima shamba

- (b) Ukimwi ni ugonjwa hatari sana
36. Tumia maneno yafuatayo katika sentensi kama vivumishi mwenyewe, kichache, enyewe.
37. Tunga sentensi zenyе vipashio vifuatavyo
- (a) W +TS+E
  - (b) N+T+V
  - (c) N+T+E
  - (d) N+TS+T+E
38. Eleza maana ya kiunganishi
39. Tunga sentensi mbili kwa kutumia kiunganishi
40. Nini maana ya vihisishi
41. Tunga sentensi mbili kwa kutumia vihisishi
42. Eleza maana ya kamusi
43. Tumia neno vizuri katika sentensi kama kivumishi
44. Taja sifa tatu za kamusi bora
45. Bainisha matumizi matano ya kamusi
46. Nini maana ya kitomeo
47. Eleza maana ya kidahizo
48. Nini maana ya mawasiliano
49. Taja mambo makuu mawili ya kuzingatia katika utoaji wa sauti
50. Eleza tanzu kuu mbili za lugha
51. Tunga sentensi mbili kwa kutumia viwakilishi vifuatavyo huyu, wao, na yule
52. Andika wingi wa viwakilishi vifuatavyo
- (a) Mimi (b) yeye (c) wewe
53. Eleza tofauti za kamatumizi za neno “barabara”
54. Eleza dhima kuu nne (4) za picha na michoro katia kamusi
55. Nomino na vielezi zinatofautianaje?
56. Ipo tofauti gani kati ya nomino na viwakilishi
57. Taja mifan miwili ya vihisishi unavyoifahamu
58. Eleza maana ya fasihi ?
59. Katika uwasilishaji wa kazi za kifasihi watu wanaosikiliza huitwa
60. Nini maana ya sanaa ?
61. Katika fasihi ufundi anaoutumia msanii kuwasilisha kazi ya fasihi hujulikana kama ?
62. Taja vipengele vitano vyta fani
63. Msanii hutumia fani kuwasilisha ujumbe au mambo ambapo mambo hayo hujulikana kama
64. Taja dhima kuu tano (5) za fasihi
65. Nini maana ya fasihi simulizi
66. Taja aina kuu mbili za fasihi
67. Toa tofauti tatu (3) kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi
68. Nini maana ya fasihi andishi
69. Taja vipengele sita vyta maudhui
70. Nini maana ya neno wahusika
71. Taja tanzu kuu nne (40 za fasihi simulizi
72. Eleza maana ya maigizo

73. Taja sifa kuu (3) tatu za fasihi simulizi
74. Nini maana ya hadithi ?
75. Tofautisha kati ya semi na ushairi.
76. Taja vipera vitano (5) vya hadithi
77. Eleza maana ya "soga"
78. Nini maana ya tarihi
79. Taja vipera vitatu vya maigizo
80. Tanzu za fasihi simulizi hugawanyika katika vikundi vidogo vidogo ambavyo hujulikana kama
81. Eleza maana ya Ngano
82. Taja vipera vitano (5) vya ushairi
83. Nini maana ya "Ngonjera"
84. Sarufi ina umuhimu gani (taja hoja 3)
85. Eleza maana ya neno silabi
86. Toa tofauti kati ya kitenzi na kielezi
87. Nini maana ya kiunganishi
88. Tunga sentensi kutokana na kielezi kifuatacho "asubuhi"
89. Taja aina tisa za viwakilishi
90. Nini maana ya nomino dhahania?
91. Tunga sentensi moja ukitumia kivumishi cha a-unganifu
92. Toa mifano miwili ya viunganishi
93. Tunga senstensi mbili tofauti kwa kutumia maneno haya (a) panga (b) kanga (c) mbuzi
94. Taja dhima kuu mbili za kamusi katika jamii
95. Eleza maana ya neno "kitomeo"
96. Taja mbinu kuu tatu za kusoma kamusi
97. Kamilisha methali ifuatayo usitukan wakunga
98. Eleza maana ya nahau zifuatazo
  - (a) Amevaal miwani \_\_\_\_\_
  - (b) Ana mkono wa biriki \_\_\_\_\_
99. Eleza maana ya vitendawili?
100. Taja faida tatu za hadithi.